## Maeneo matatu ya Kipaumbele

### 1. Ukuaji wa Kiuchumi

**Maendeleo ya kilimo** yamekuwa yakipewa kipaumbele katika ushirikiano wa JICA na Serikali ya Tanzania katika muda wa miaka 50 iliyopita. Ushirikiano wa JICA, hasa katika zao la mpunga kupitia kilimo cha umwagiliaji, ulianzia Mkoa wa Kilimanjaro, na hadi sasa umeenea nchi nzima pamoja na Zanzibar.

Katika sekta ya **maendeleo ya viwanda**, JICA inatoa msaada wa kiufundi kwenye viwanda vidogo na vya kati kwa lengo la kuboresha menejimenti na tija katika viwanda hivyo.







### 2. Maendeleo ya Miundombinu

JICA imekuwa mmoja wa wabia wakubwa katika maendeleo ya miundombinu, hasa katika sekta ndogo za **uchukuzi** na **umeme**. Msaada huu umelenga maeneo ya mijini ambako mahitaji ni makubwa zaidi. Msaada huo ni pamoja na kujenga na kutengeneza miundombinu mbalimbali (facilities) kwa kutumia misaada bila masharti na mikopo ya ODA, na kuboresha mfumo wa utunzaji na utawala kwa kutumia ushirikiano wa kiufundi.

Katika sekta ya **maji** JICA inasaidia katika upatikanaji wa maji safi na salama kwa watu wa vijijini na pia kuhamasisha utumiaji uendelevu na wenye manufaa wa vyanzo vya maji ambavyo ni vichache.







### 3. Uboreshaji wa Huduma za Umma

JICA imekuwa inasaidia jitihada za serikali ya Tanzania katika **maboresho ya serikali za mitaa** na katika uimarishaji wa uwezo wa sekta ya **umma katika eneo la utawala na utunzaji wa kifedha,** lengo likiwa ni kuwezesha utoaji wa huduma za umma zilizo bora, za haki na za usawa kulingana na matakwa ya wananchi.

JICA imekuwa inajishughulisha na uimarishaji wa manejimenti ya utawala wa afya kitaifa na kimikoa kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma kwa wananchi. Zaidi ya hayo, JICA inasaidia katika elimu ya shule na mafunzo ya kiufundi kwa kutuma wafanyakazi wa kujitolea.












Japan International Cooperation Agency
3rd Floor, Barclay's House, 1008/1 Ohio Street,
S. L. P. 9450, Dar es Salaam, Tanzania
Simu +255-22 211 3727~30
Nukushi +255-22 211 2976
http://www.jica.go.jp/tanzania/english/index.html










# JICA TANZANIA



## Maendeleo ya Kasi na Kwa Wote

Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japani (JICA) ni shirika huru la kiserikali ambalo linaratibu misaada rasmi inayotolewa na Seikali ya Japani (ODA). JICA ni shirika kubwa la kitaifa la msaada kuliko yote duniani, na linafanya kazi katika nchi na sehemu zaidi ya 150 na lina ofisi 100, kati ya hizo 34 ziko katika nchi za Afrika, Tanzania ikiwamo.

Ushirikiano wa Japani na Tanzania ulianza mwaka 1962. JICA inafanya kazi pamoja na Serikali ya Tanzania kwa ajili ya maendeleo na furaha ya watu wake.

## Matunda ya JICA katika Tanzania kwa miaka 50

| | |
|---|---|
| Ushirikiano wa Kiufundi 1259 Billion Tsh | Wataalamu 1300 wa JICA wameletwa tangu 1965 |
| | Watanzania 3200 walihudhuria mafunzo Japani tangu 1962 |
| Mikopo ya ODA 876 Billion Tsh | Mifano: Barabara, Daraja, Umeme, msaada kwa bajeti ya Taifa |
| Misaada bila Masharti 2856 Billion Tsh | Mifano Barabara, Daraja, Umeme, Maji, Soko la samaki, Shule n.k. |
| Japan Overseas Cooperation Volunteers 234 Billion Tsh | Wafanyakazi 1400 wa kujitolea wa JICA tangu 1967 |

(Takwimu ni za 2010 – kiwango cha kubadilisha pesa 18 Tsh/JP yen) (Takwimu ni za 2012)

## Miradi inayoendelezwa na JICA Tanzania kwa sasa (mifano kadhaa ya 2013)

### Shinyanga
JICA inafadhili mradi kwa ajili ya kuimarisha huduma ya afya ya mama na mtoto - mradi ambao unaendeshwa na asasi mbili za kiraia, JOICFP (Japani) na UMATI (Tanzania). Watoaji huduma waliochaguliwa na wanavijiji wanafundishwa.

### Arusha
Kupitia mkopo wa ODA, JICA inatoa msaada wa kifedha kwa kuboresha barabara ya Arusha-Namanga-Athi River ambayo inachangia katika uboreshaji wa mtandao wa usafiri kati ya Tanzania na Kenya, na nchi nyingine zaidi.

### Kilimanjaro
Japani ilisaidia kujenga skimu ya umwagiliaji katika Lower Moshi miaka ya 1970. Tangu wakati huo wataalamu wa kilimo wajapani wamesaidia vituo vya mafunzo ya kilimo Kilimanjaro na sehemu nyingine kwa kuendesha mafunzo ya wakulima. Kutokana na hayo wakulima wameongeza mavuno katika sehemu nyingi.

### Zanzibar
JICA inasaidia kuboresha miundombinu ya maji katika eneo la mji wa Zanzibar. Kwa kudumisha miundombinu hiyo, JICA inasaidia Mamlaka ya Maji Zanzibar kuboresha utawala wake kwa kuimarisha uwezo wa kutumia maji na kutunza fedha vizuri.




### Dar es Salaam
JICA inasaidia maendeleo ya wafanyakazi katika TANESCO, kwa lengo la kuimarisha mtandao wa kusafirisha na kusambaza umeme kwa kupitia mafunzo ya wahandisi na mafundi. Wafanyakazi wapatao 2100 watafundishwa utunzaji mzuri wa miundombinu ya TANESCO.

### Dodoma/Iringa
Mradi wa Maendeleo ya Mfumo wa Kutunza Barabara za Vijijini unalenga kuboresha utendaji wa wahandisi wa wilaya katika upangaji, ununuaji, utekelezaji, na uthamini wa utunzaji/maendeleo ya barabara za vijijini.

### Morogoro/ Pwani/ Dodoma
JICA inatoa msaada wa kiufundi kwa kuanzisha mfano mzuri wa O & OD ambao ni mchakato shirikishi wa maendeleo ya jamii kama ulivyoainishwa katika Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa.